# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MAADHIMISHO YA KWANZA YA *WIKI YA USAFIRI ENDELEVU WA ARDHINI 2025,* DAR ES SALAAM, NOVEMBA 24 HADI 29, 2025

***Dar es Salaam, 29 Agosti, 2025***

Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeandaa maadhimisho ya kwanza ya **Wiki ya Usafiri Endelevu wa Ardhini 2025** inayotarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam, Novemba 24 hadi 29, 2025. Wiki hii itaadhimishwa Nchini Tanzania kuunganana na Nchi nyingine duniani kutambua **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani** (World Sustainable Transport Day) tarehe **26 Novemba kila mwaka**.

Katika Azimio Na. 77/286 la tarehe 16 May 2023, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN General Assembly) liliazimia kila mwaka tarehe Novemba 26 iwe ni **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani (World Sustainable Transport Day)** na kuzikaribisha Nchi zote duniani, Taasisi za Umoja wa Mataifa, Taasisi za Kikanda na Kimataifa, Jumuiya za Kiraia, ikijumuisha Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs), na wadau wengine wote wa usafiri na usafirishaji, kuiadhimisha siku hii kwa kutoa elimu na kuandaa shughuli zitakazokuza elimu juu ya masuala ya usafiri na usafirishaji, hususan aina za usafiri bora na salama, kuhamasisha usafiri unaotunza mazingira, kujenga miundombinu ya usafiri inayozingatia watu wenye mahitaji maalum, na masuala mengine ya usafiri bora, salama na endelevu.

Hivyo, ili kutekeleza vyema Azimio hili la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, na kwa kutambua na kuunga mkono juhudi za Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi, Serikali kupitia LATRA imepanga kuadhimisha Wiki ya Usafiri Endelevu wa Ardhini, Novemba 24 hadi 29, yenye Kauli Mbiu ***Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji (Green Transport and Innovation).*** Kaulimbiu hii inasisitiza jukumu muhimu la mifumo ya usafiri shirikishi, yenye ustahimilivu na iliyo rafiki kwa mazingira katika kufanikisha **Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia.** Kutokana na umuhimu wa siku hii, tunatarajia Mgeni Rasmi atkuwa Mheshimiwa Rais mwenyewe.

**Ndugu wanahabari,**

Maadhimisho ya **Wiki ya Usafiri Endelevu wa Ardhini 2025** itajumuisha **makongamano, midahalo ya kisera, maonesho na mengineyo** - ikileta pamoja washiriki kutoka Tanzania Bara na Visiwani, na ukanda mzima wa Afrika Mashariki na Jumuia ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC) ili kuunda mfumo wa usafiri wa ardhini ulio **bora zaidi, wenye ufanisi, tija na endelevu.** Maadhimisho haya yatahusisha **usafiri wa barabara, usafiri wa reli, na usafiri wa waya** kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mnafahamu kwamba **Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga Duniani** huadhimishwa kila mwaka tarehe **07 Desemba** na hapa Nchini, **Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA)** husimamia maadhimisho hayo chini ya miongozo ya **Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO).** Aidha, **Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Majini Duniani** huadhimishwa kila mwaka tarehe **26 Septemba** na hapa Nchini, **Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)** husimamia maadhimisho hayo chini ya miongozo ya **Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO)**. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongoza Taifa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na inayotambu maazimio ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, imeamua kupitia Wizara ya Uchukuzi na LATRA, kuanzia mwaka 2025 tuanze kuiadhimisha rasmi Siku ya Usafiri Endelevu Duniani, kwa jina la **Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini**.

**Ndugu wanahabari,**

Lengo la maadhimisho haya ni kuwaleta pamoja wadau wa sekta ya usafiri ardhini, kujadili na kuweka malengo ya pamoja ya utekelezaji juu ya namna bora ya kuboresha sekta ya usafiri ardhini ili iwe na tija kwa watoa huduma, watumia huduma, Serikali na jamii kwa ujumla. Aidha, maadhimisho hayo yanalenga kuhamasisha matumizi ya nishati safi kwa mazingira pamoja na kuhimiza ubunifu na matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, pia kutambua na kuweka mikakati ya kuwa na miundombinu yenye kuzingatia watu wenye mahitaji maalum katika sekta ndogo za **usafiri wa barabara**, **usafiri wa reli na usafiri wa waya**. Vilevile, maadhimisho haya yanalenga kukuza ushindani na ufanisi baina ya watoa huduma za usafiri ardhini, hususan wasafirishaji, kuhamasisha uwekezaji, ushirikiano, kupanua wigo wa uboreshaji wa huduma za usafiri ardhini pamoja na kuhamasisha watoa huduma za usafirishaji kutekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Sheria Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini nchini.

Kwa ujumla, maadhimisho haya yataambatana na makongamano na mijadala itakayofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), pia kutakuwa na maonesho kutoka kwa wadau kutoka Serikalini, Taasisi za Umma Nchini, na Sekta Binafsi ndani na nje ya nchi. Huduma na fursa mbalimbali zitatolewa kwa wadau watakaoshiriki ikiwa ni pamoja kuunganisha wadau katika fursa mbalimbali za kibiashara, kuongeza mtandao wa biashara na maonesho ya ubunifu katika huduma mbalimbali za usafiri ardhini.

**Ndugu wanahabari,**

Maadhimisho ya Wiki ya Usafiri Endelevu wa Ardhini yatahitimishwa tarehe 29 Novemba 2025 kwa kutoa tuzo mbalimbali. Wizara ya Uchukuzi kupitia LATRA, ilianza kutoa Tuzo za Wasafirishaji Bora na Salama mwaka 2024 ambazo zilitolewa kwa washindi na Mhe. Dkt Philip Isdori Mpango, jinini Dodoma, katika maadhimisho ya Wiki ya Usalama Barabarani 2024. Kwa sasa, Wizara ya Uchukuzi kupitia LATRA, inaratibu TUZO za Watoa Huduma Bora za Usafiri wa Umma kwa mwaka 2025. Tuzo hizi zitatolewa kwa watoa huduma wa usafirishaji wa abiria, mizigo, pamoja na mifumo inayochangia mnyororo wa thamani wa sekta ya usafiri wa umma, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Juni 2025**. Aidha tuzo maalum zitatolewa kwa wadhamini wa maadhimisho kulingana na viwango vya udhamini uliotolewa.**

**Tuzo hizi zitawalenga;**

- Wasafirishaji kwa malori yanayotoa huduma ya usafirishaji wa mizigo ndani ya nchi na nje ya nchi
- Wasafirishaji kwa mabasi masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani)
- Madereva wa Mabasi ya masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani)
- Wahudumu wa Mabasi ya masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani)
- Watoa huduma za mifumo ya tiketi
- Watoa huduma ya Mifumo ya Ufuatiliaji Mwenendo wa Magari (VTS)
- Watoa huduma ya mifumo ya Teksi mtandao
- Watoa huduma za Usafiri wa Waya (Cable Transport)
- Wanahabari na wadau walioonesha mfano wa kuigwa katika kuhamasisha umma kuhusu huduma bora za usafiri ardhini

Kwa upande wa huduma za usafiri, kura za watumiaji huduma zitachangia alama 40 katika ya 100 za ushindi wa jumla wa mshindani.

Abiria na wadau wa kawaida watawezeshwa kushiriki kwa kujaza dodoso linalopatikana kwenye tovuti ya Maadhimisho, Dodoso la kimtandao na tovuti ya LATRA www.latra.go.tz, pamoja na mitandao ya kijamii. **Taarifa zaidi juu ya utaratibu wa kushiriki na kuwapigia kura washiriki zitatolewa ndani ya mwezi Septemba, 2025.**

**Ndugu wanahabari,**

Kwa ujumla, Maadhimisho ya Wiki ya Usafiri Endelevu wa Ardhini ni jukwaa zuri la wadau kujifunza, kujengeana uwezo, kutambua juhudi na kufahamu mifumo ya TEHAMA inavyosaidia kuboresha sekta ya usafiri ardhini, kubadilishana uzoefu na kupata fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji kipindi chote cha maadhimisho haya. Wananchi wote, taasisi za serikali, sekta binafsi, wanafunzi, watafiti, na wadau wa usafiri mnakaribishwa kuunga mkono juhudi hizi kupitia kudhamini maadhimisho hayo, kushiriki kuonesha bidhaa na huduma na kushiriki katika makongamano yatakayoandaliwa.

**Ndugu wanahabari,**

Mwisho, sio kwa umuhimu, naomba nitumie fursa kukushukuruni sana ndugu wanahabari kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kutoa elimu, kuhabarisha umma, na kwa ujumla, mmekuwa mabalozi wema na mahiri kwa umma. Tunatambua na kuthamini sana thamani ya kalamu zenu, niwaombe katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu 2025 kuandika taarifa zitakazodumisha umoja, mshikamano na upendo miongozi mwa watanzania. Tuweke mbali tofauti zetu za kiitikadi na tulinde amani ya Taifa letu kwa kutumia kalamu zetu, na kauli zetu.

*Asanteni kwa Kunisikiliza*

**CPA Habibu Juma Suluo**

**MKURUGENZI MKUU - LATRA**